# OFISI YA RAIS

# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MANISPAA YA KINONDONI, WILAYA YA BAGAMOYO, KIBAHA MJI (KIBAKI)

## MTIHANI WA PAMOJA, 2023

## NSIMB0:015 ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

**MUDA: 3 Hours** **MWAKA:2023**

**Maelekezo**

1. Mitihani huu una A, B na C zenye ju mla ya naswali kumi na moja (11)
2. Jibu maswali yote katika kila sehemu
3. Sehemu A ina alama kumi na sita (16), sehemu B ina alama hamsini na nne (54) na sehemu C ina alama thelathini (30)
4. Zingatia maelekezo ya kila sehemu nay a kila swali
5. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani
6. Andika namba yako ya mtihani katika kila ukurasa wa kitabu chako cha kujibia
7. Zingatia maelekezo ya kila sehemu nay a kila swali
8. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani
9. Andika namba yako ya mtihani katika kila ukurasa wa kitabu chako cha kujibia

**SEHEMU A (ALAMA 16)**

**Jibu maswali yote katika sehemu hii**

1. Chagua jibu sahihi katika kipengele cha (i)-(x), kisha andika herufi ya jibu hilo kwenye kijitabu chako cha kujibia

i. "Na Mwenyezi Mungu akamfundisha Adam majina ya vitu vyote" katika aya hii majina ya vitu vyote ina maanisha

A. Kusoma majina ya watu na vitu vinavyowazunguka
B. Fani zote za elimu ambazo anazihitaji mwanadamu hapa duniani kufikia lengo la kuumbwa kwake
C. Kutekeleza sharti la Mwenyezi Mungu la kutafuta elimu
D. Kuyajua maumbo mbalimbali ulimwengu na kuyatumia
E. Kumtukuza Allah (sw) katika ugawaji wake wa elimu na vipawa

ii. Ni mafunzo yapi tunayapata kutoka kwenye hadithi ya mtume (sw) isemayo "Yule ashikae upanga (silaha) dhidi yetu si pamoja na sisi"

A. Muislamu kushika upanga
B. Muislamu wa kweli hawezi kumdhuru muislamu mwenzake
C. Muislamu mwenye upanga asifuatane na Mtume (saw)
D. Kila anayeshika upanga anapaswa kuuwawa
E. Anapokaa Mtume (saw), maswahaba hapaswi kushika upanga

iii. Katika maandalizi ya Ki-ilhamu aliyopewa Mtume (saw) kabla ya kupewa rasmi utume kuna mengi yakujifunza. Moja wapo ya funzo tupatalo ni;

A. Elimu katika kuongoza jamii ni jambo la msingi sana
B. Kupewa utume si kazi na jambo la kibubusa
C. Hatuna budi kuwaandaa watoto wetu kuwa makhalifa wa Allah (sw)
D. Kujitenga kwenye pango kama alifanya mtume (sw)
E. Kuchunga mbuzi na kondoo kunamfanya kiongozi kuwa na subra

iv. Qiyas na Ijumaa ni misingi miwili iliyotumika katika kumpata khalifa yupi baada ya Mtume (saw) kutawafu?

A. Ali bin Abi twalib
B. Umar bin khatwah
C. Abdullah bin Umar
D. Abubakari swiddiq
E. Uthmani bin Affaan

v. "Kwani hukuona jinsi mola wako mlezi alivyowanya kina A'di? wa Iram wenye majumba marefu" (89:67). Yupi katika mtume wafuatao alikuwa wa umma wa Adi?

A. Yunus (AS)
B. Nuhu (AS)
C. Ibrahim (AS)
D. Mussa (AS)
E. Swalehe (AS)

vi. Kwa Mwenyezi Mungu hakuna jambo linalotokea kwa ghafla au bahati mbaya, bali kila tukio baya au zuri lipo katika milki ya Allah (sw). Kwa mujibu wa Imani ya kiislam kauli hii ina maanisha

A. Kuamini Mwenyezi Mungu na mitume wake
B. Kuamini malaika walete adhabu kwa wanadamu
C. Kuamini nguzo ya sita ya Imani ya kiislam
D. Kuamini wanazuonie wanaosemea na kuondoa mabalaa
E. Kuamini nguzo ya kwanza ya Imani ya kiislamu

vii. Moja kati ya mambo yafuatayo humuwajibisha mwanadamu kufuata dini sahihi katika maisha yake

A. Kuwepo kwa dini nyingi duniani
B. Kuletwa kwa mitume wa Mwenyezi Mungu
C. Kuwepo kwa midahalo ya kidini
D. Uwezo wa mwanadamu kuamua
E. Hitajio la mwanadamu kiroho

viii. Ibada gani kati ya zifuatazo humuandaa mja kumpenda Allah (sw) kuliko chochote katika ulimwengu hata kuliko nafsi yake?

A. Kuhiji Makkah
B. Kutoa zakah na sadaka
C. Swala za faradhi
D. Kutoa shahada mbili
E. Kufunga mwezi wa ramadhani

ix. Msisitizo wa kuanza kila jambo jema kwa Bismillah ni hadithi ya Mtume (SAW) lakini ni funzo linalopatikana kwenye sura

A. An Naas
B. Al kauthar
C. Al ikhlaas
D. Al faatiha
E. An Nasr

x. Anapaswa afanye nini mtu anayemsalia maiti baada ya kuleta takbira ya nne?
   A. Kumuombea maiti
   B. Kuwaombea dua waislam
   C. Kusoma suratul – fa'atiha
   D. Kusoma swala ya Mtume (SAW)
   E. Kutoa salaamu

2. Oanisha matendo ya ibada ya hijjah kwenye orodha A na maana zake zilizopo katika orodha B ili kupata maana iliyokusudiwa

| ORODHA A | ORODHA B |
|---|---|
| i. Ihram | A. Ni kitendo cha mahujaji kupiga kambi mina na kulala hapo hadi asubuhi kuelekea arafa |
| ii. Talbiya | B. Ni kitendo cha mahujaji kutembea mara saba baina ya vilima viwili vya saffaa na Mar'waa |
| iii. Tawaf | C. Ni kitendo cha mahujaji kusimama tangu swala ya adhuhuri baina ya vilima vitatu katika bonde la arafa hadi magharibi na kuomba dua mbalimbali |
| iv. Sai | D. Ni kitendo cha mahujaji kuzunguka ka'aba baada ya kumakamilika kwa ibada ya hijjah |
| v. Tawaful widaa | E. Ni kitendo cha mahujaji kuwa katika vazi rasmi na miiko kwaajili ya hijjah au umrah |
| vi. Kisimamo cha arafa | F. Ni kitendo cha mahujaji kuitikia wito wa Mwenyezi Mungu (SW) kwa kutamka maneno rasmi ya mahujaji |
| | G. Ni kitendo cha kuizunguka ka'abu mara saba kwa mwelekeo wa kinyume na saa na kulibusu au kuligusa au kwa kuashiria |
| | H. Ni kitendo cha mahujaji kunyoa nywele, kuchinja mnyama na kutupa mawe kwenye minara mitatu |

**SEHEMU B (ALAMA 54)**
**Jibu maswali yote katika sehemu hii**

3. (a) Abu Harairah (R.A) amesimulia kuwa mtume (SAW) amesema "Mwanamke anaolewa kwa vitu (sifa) vinne….". Kamilisha hadithi hiyo ya Mtume (SAW) kwa kuvitaja hivyo vitu (sifa) vinne.
   (b) Kwa kutumia nukta tano (5) ielimishe jamii juu ya lengo la ndoa katika uislamu

4. (a) Ni kwa namna gani Dola ya kiislamu aliyoianzisha mtume (SAW) madina iliporomoka? (Toa hoja tatu)
   (b) Ukiwa mwanafunzi wa kiislamu unajifunza nini kutokana na kuporomoka kwa dola ya kiislamu Madina (Toa hoja tatu)

5. "Wale walao riba hawasimami ila kama anavyosimama aliyezugwa na shetani kwa kumgusa"….. (2:275). Ukiwa msomi wa dini ya kiislamu tumia nukta sita (06) kuizindua jamii ya sasa juu ya uharamu wa riba

6. (a) Kuwatii wazazi wawili ni jambo lililosisitizwa sana katika Qur'an na Sunnah za mtume (saw). Bainisha wajibu wa watoto kwa wazazi wao. (Toa hoja tano)

(b) Eleza ni kwa namna gani Tawhiid inaweza kutumika katika kusimamisha haki katika jamii

7. Mkataba wa hudaybiyya ulikuwa mwiba mchungu kwa maswahaba kutokana na masharti yake magumu kwa waislamu, na baadaye ulileta ushindi mkubwa katika Dola ya kiislamu. Kwa kutumia hoja sita (06) chambua mafanikio yatokanayo na mkataba huo.

8. (a) Kila mwanadamu ni mwenye kufanya makosa, na mkosaji mzuri ni yule mwenye kufanya toba ya kweli. Bainisha masharti matano (5) ya toba ya kweli.

(b) Toa udhaifu wa dai linalosema kuwa hapana uwezekano wa kupatikana uhai baada ya mtu kufa, kuoza na kusagikasagika (79:10)

**SEHEMU C (ALAMA 30)**

**Jibu maswali mawili (2) tu katika sehemu hii**

9. Qur'an ni muongozo kamili wa maisha ya mwanadamu katika Nyanja zote za maisha, na atakae ifuata kikamilifu kwa hakika amepata uongofu mkubwa duniani na akhera. Tumia hoja tano (5) kuwaeleza waislamu wa leo kwa nini pamoja na kuisoma Qur'an bado athari yake haionekani katika maisha yao ya kila siku.

10. Waislamu wengi wa siku hizi hawaswali kwa wakati na wanapoulizwa hudai wataswali "Kadha". Eleza madhara mawili (2) anayoyapata muislamu kwa kutoswali kwa wakati na utoe mapendekezo matatu ya nini kifanyike ili kuipa hadhi swala kwa muislamu.

11. Historia ya ukusanyaji na uandishi wa hadithi za mtume (SAW) ulipitia katika hatua nne za msingi. Eleza kila hatua na namna hadithi zilivyoandikwa kwa wakati huo.

*- * Wabillah Tawfiq **